**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MAJI**

**WAKALA WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJ**

Ofisi ya Meneja wa Mkoa, S.L.P 1129, Musoma - Mara,
**Simu**: +255(0) 737 874 168, **Tovuti**: www.ruwasa.go.tz
**Baruapepe**: mararm@ruwasa.go.tz

# MKATABA MDOGO WA AJIRA ZA MAFUNDI

**KATI YA**

**MENEJA WA RUWASA MKOA WA S.L.P 1129, MUSOMA - MARA**

**NA**

**FUNDI UJENZI PATROBERT MAGEGE WA S.L.P 898 MUSOMA**

**KWA**

**UJENZI WA VITUO 7 VYA KUCHOTEA MAJI NA KIOSKI 1 MRADI WA MAJI BUGOJI/KABURABURA/KANDEREMA.**

**MKATABA NA. : RUWASA/MARA/MUSOMA/BUGOJI/COVID/2021-2022/03**

**JANUARI, 2022**

**FOMU F2**

**MKATABA WA UJENZI WA VITUO 7 VYA KUCHOTEA MAJI NA KIOSKI 1**

**MKATABA HUU** unafanyika leo tarehe ...31..... mwezi .....01..... mwaka 2022

**BAINA YA**

**WAKALA WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA (RUWASA), MKOA WA MARA S.L.P 1129, MUSOMA - MARA** (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiri au RUWASA") kwa upande mmoja;

**NA**

Ndugu PATROBERT MAGEGE. wa **S.L.P** 898 MUSOMA (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiriwa au Fundi") kwa upande mwingine.

**KWAMBA** kwa pamoja Mwajiri na Mwajiriwa watajulikana kama pande mbili za Mkataba.

**AMBAPO:**

a) Mwajiri ni Wakala wa Serikali wenye jukumu la kutekeleza ujenzi wa miradi ya maji vijijini na kusimamia utoaji wa huduma ya maji na usafi wa mazingira vijijini na yenye makao makuu yake Jijini Dodoma;

**b)** Mwajiriwa ni mtu binafsi anayefanya shughuli zake binafsi za ujenzi

c) Mwajiri anakusudia kumwajiri Mwajiriwa kwa kipindi cha muda mfupi wa siku .........;

Mwajiriwa anakubali matakwa ya Mwajiri na anakubali kwa hiari yake mwenyewe kuajiriwa kwa muda mfupi kama FUNDI UJENZI VITUO VYA KUCHOTEA MAJI

**MKATABA HUU UNASHUHUDIA** kwa pande zote mbili kukubaliana kama ifuatavyo:

## 1. MADHUMUNI YA MKATABA

Mkataba huu ni kwa ajili ya UJENZI WA VITUO 7 VYA KUCHOTEA MAJI NA KIOSKI 1

Ambapo Mwajiriwa atapaswa kufanya kazi zote kama zilivyoambatanishwa kwenye makadirio ya kazi BOQ (**makadirio ya kazi BOQ imeambatanishwa**)

**NB:** *Ujenzi huo utajengwa kwa kuzingatia michoro na maelekezo kutoka kwa mwajiri.*

## 2. MUDA WA UTEKELEZAJI WA KAZI

Kazi hii itafanyika kwa muda wa siku ........ ambapo itaanza tarehe ....../....... /............ na itakamilika tarehe ....../....../2022.

Kushindwa kukabidhi kazi hiyo ndani ya muda tajwa Mwajiri ana uwezo wa kuvunja mkataba ndani ya siku ........ baada ya tarehe ya mkataba kumalizika'

## 3. ONGEZEKO LA MUDA WAUTEKELEZAJI KAZI

i. Kwamba mwajiriwa ana haki ya kuwasilisha ombi la muda wa nyongeza kwa mwajiri wake akitaja sababu zinazopelekea muda kuongezeka

ii. Mwajiri atatafakari kwa kina ombi la mwajiriwa(fundi) na kutoa maamuzi yake bila kuingiliwa akitaja sababu za kuongeza au kutokuongeza muda wa utekelezaji endapo kama sababu ni sahihi au sio sahihi bila kuathiri gharama na muda wa mkataba

iii. Mwajiriwa (fundi) anayo haki ya kuomba ongezeko la muda wenye tija na vifaa kwa ajili ya kutekeleza mabadiliko ya kimkataba kama upo ushahidi wa ongezeko ili kazi yote pamoja na mabadiliko ikamilike kwa ufanisi kwa taratibu za kiufundi.

## 4. MUDA WA MATAZAMIO

Mwajiriwa (fundi) atahakikisha anafanya marekebisho ya hitilafu zozote na kufanya mradi salama kipindi chote cha matazamio ya siku .......... tangu tarehe ya kukamilisha kazi ndipo apewe hati ya ukamilishaji wa kazi na kuacha eneo la kazi safi na salama.

## 5. MABADILIKO MADOGO YA KAZI,KUONGEZEKA NA KUPUNGUA KWA KAZI

**i.** Mwajiri kupitia kwa msimamizi wa kazi (Meneja mradi) ambaye ni Meneja wa Wilaya anayo haki ya kufanya mabadiliko ya aina yoyote pamoja na kuongeza au kupunguza kazi ndani ya asilimia 15 **(15%) kwa kibali cha barua toka kwa mwajiri mwenyewe, taratibu zote mabadiliko na si vinginevyo.**

ii. Mwajiriwa (fundi) atalazimika kuweka bei ya kazi ndogo ambazo zimeongezeka na ambazo viwango vyake (rates) hazipo katika makadirio ya kazi ya awali (BOQ) lakini kwa kazi ambazo zinapungua au kuongezeka na zipo ndani ya makadirio ya awali ya mkataba,bei halisi itapatikana kwa kutumia viwango vilivyo katika makadirio hayo ya kazi (BOQ) na si vinginevyo hata hivyo mabadiriko yoyote hayatakubaliwa bila mapatano ya kimaandishi kati ya pande zote mbili.

## 6. MALIPO YA UTEKELEZAJI WA KAZI

Mwajiriwa atalipwa jumla ya kiasi cha **TShs 5,042,000.000** Kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu;

a) Malipo ya Mwajiriwa yatakuwa ni kwa fedha za kitanzania tu (*Tanzanian Shillings*);

b) Malipo hayo yatalipwa aidha kwa fedha taslim au hundi ambayo italipwa benki;
c) Malipo ya Mwajiriwa yatalipwa kwa kuzingatia ubora na kiasi cha kazi zilizofanyika na kukamilika kwa mujibu wa BOQ iliyojazwa.
d) Malipo ya Mwajiriwa yatalipwa mara baada ya kukamilisha kazi ya ujenzi kama ilivyoainishwa katika kifungu **1** kifungu kidogo **(a)** kwa utaratibu ufuatao;
    - Malipo ya awali yatalipwa asilimiaa **20%** baada ya ukamilifu wa kazi usiopungua asilimia **20%**.
    - Awamu ya pili (2) yatalipwa asilimia **30%** baada ya ukamilifu wa kazi usiopungua asilimia **65%**.
    - Awamu ya tatu (3) Asilimia **30%** baada ya ukamilifu wa kazi usiopungua asilimia **95%**.
    - Awamu ya nne (4) Asilimia **10%** baada ya ukamilifu wa kazi kwa asilimia **100%**.
e) Kwamba kama fundi mjenzi ana uwezo wa kutosha kutekeleza kazi hiyo pasipo kuomba malipo yoyote katika mchaganuo tajwa hapo juu anaweza kufanya kazi yote kwa ukamilifu na ubora kisha kuomba malipo yote kwa mara moja baada ya kazi kukamilika,kukaguliwa na kukubalika na mwajiri.
f) Kabla ya malipo ya mwisho kufanyika,Mwajiriwa anapaswa kuwasilisha taarifa zote zinazohitajika na kufanya marejesho ya vifaa vyote vya kazi na fedha za mradi kama zitakuwepo.

## 7. HAKI NA WAJIBU WA MWAJIRI

Mwajiri ambaye atawakilishwa na Msimamizi wa Kazi, atakuwa na wajibu na majukumu yafuatayo:

a) Kutoa baadhi ya vifaa kwa ajili ya ujenzi wa kazi hii;
b) Kusimamia na kuthibitisha ubora wa kazi inayofanywa na fundi;
c) Kuwasiliana na uongozi wa eneo husika namna ya kuwashirikisha wananchi/Jumuiya ya Watumia Maji katika shughuli za ujenzi wa Mradi;
d) Endapo kazi itakayofanywa na Mwajiriwa haitafikia viwango vya ubora unaotakiwa, Mwajiri atachukuwa hatua stahiki dhidi ya Mwajiriwa huyo; na Msimamizi wa Mradi ata mtaarifu fundi wa kazi hii kwamba ameshindwa kutimiza masharti ya makubaliano.
e) Kuhakikisha kuwa endapo Mwajiriwa atafanya kazi isiyokidhi viwango au isiyoridhisha, Mwajiriwa huyo anarekebisha au kurudiwa upya kazi hiyo kwa gharama zake mwenyewe.

## 8. HAKI NA WAJIBU WA MWAJIRIWA

Mwajiriwa ambaye ni fundi atakuwa na wajibu na majukumu yafuatayo:

a) Kuhakikisha kuwa anatekeleza ujenzi wa kazi zote kama zilivyoelekezwa kwenye sehemu ya 1 (Madhumuni ya Mkataba) kulingana na ramani na vipimo viliyotolewa na Mwajiri;
b) Kuhakikisha kuwa anawajibika kufanya kila jambo ambalo kwa ujumla wake litaleta mafanikio kwenye mradi atakaoujenga;
c) Atatekeleza majukumu yake kwa uaminifu, uadilifu, umakini na weledi mkubwa na endapo atatekeleza kinyume na matakwa haya, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake;
d) Atawajibika kwa Msimamizi wa Mradi (*Project Manager*) kwa utendaji wake wa kila siku na atatekeleza maelekezo anayopewa na kiongozi huyo;
e) Atawajibika kuhudhuria mikutano ya tathmini ya mradi pamoja na watendaji wengine wa timu yake kila itakapopangwa;
f) Atawajibika kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa mradi kila zitakapohitajika;
g) Kuhakikisha malipo ya vibarua na mafundi walioajiriwa kwa mikataba midogo yanafanyika kwa wakati; na
h) Kufanya usafi eneo la ujenzi wa mradi na kuondoa mabaki yote ya vifaa vya ujenzi na kuviweka katika eneo litakaloelekezwa na Msimamizi wa Mradi.

## 9. HAKI NA WAJIBU WA JUMUIYA YA WATUMIA MAJI/WANANCHI

Jumuiya ya Watumiaji Maji itakuwa na wajibu na majukumu ya fuatayo:

a) Kushiriki katika kazi ndogo ndogo za kujitolea kwa ajili ya kushirikiana na mafundi;
b) Kutekeleza majukumu mengine pale inapohitajika kwa maelekezo ya Msimamizi wa Mradi; na
c) Kulinda vifaa vya ujenzi, mitambo na mradi wenyewe ili usihujumiwe.

## 10. UTOAJI WA MIKATABA MIDOGO

Mwajiriwa anaweza kuingia Mikataba midogo kiasi kadhaa ya utekelezaji wa kazi na vibarua (*casual labourers*) watakaokuwa chini ya usimamizi wake.

## 11. UCHELEWESHAJI WA UTEKELEZAJI WA MRADI

Endapo kazi haitakamilika katika muda uliopangwa, Mwajiriwa atalipa faini ya asilimia **(0.01%)** ya malipo ya kazi yote kwa kila siku ya ucheleweshwaji isipokuwa kukiwa na sababu ya msingi ya ucheleweshwaji wa kazi ulioidhinishwa kwa maandishi na Msimamizi wa Mradi.

## 12. DHAMANA YA UHARIBIFU

a) Mwajiriwa atawajibika kulipa gharama za uharibifu au madhara yoyote yatakayosababishwa na wafanyakazi wake au vifaa vyake wakati wa utekelezaji wa mradi; na

b) Gharama hizo au madhara hayo yatabainishwa na Msimamizi wa Mradi kwa maandishi.

## 13. SHERIA ITAKAYOTUMIKA

Mkataba huu utaongozwa na kusimamiwa na Sheria za Tanzania.

## 14. USULUHISHI WA MGOGORO

Endapo kutatokea mgogoro wa aina yoyote baina ya Mwajiri na Mwajiriwa kuhusu utekelezaji wa mradi huu:

a) Pande zote mbili zitatatua mgogoro huo kwa njia ya amani ya mazungumzo ambapo makubaliano ya pande hizi mbili yatapelekea Mkataba huu kufanyiwa marekebisho; na
b) Endapo mgogoro huo utashindikana kutatatuliwa kwa njia ya amani ya mazungumzo, pande zote mbili zinaweza kuchukua hatua stahiki za kisheria kwa mujibu wa Sheria za Tanzania.

## 15. KUSITISHA MKATABA

Mkataba huu unaweza kusitishwa endapo upande mmoja au pande zote mbili za Mkataba zitashindwa kutekeleza wajibu wake au masharti ya Mkataba huu.

## 16. MAREKEBISHO YA MKATABA HUU

Kwamba Mwajiri na Mwajiriwa wanaweza kubadilisha baadhi ya masharti ya Mkataba huu kwa makubaliano ya pamoja kwa njia ya maandishi.

## 17. MASHARTI YA NYONGEZA

Masharti mahsusi ya nyongeza kuhusiana na utekelezaji wa mradi huu ni pamoja na:

a) Mwajiriwa awe na uwezo wa kufanya kazi kwa asilimia **20%** bila kuomba malipo.
b) Hakuna malipo ya awali (advance)

**KWA USHUHUDA HUU**, pande zote mbili zinaweka sahihi zao katika Mkataba huu siku na tarehe kama ilivyooneshwa hapa chini:

**KWANIABA YA MWAJIRI (RUWASA)**

**Jina:** Tulinumpoki Mwakalukwa

**Sahihi:** [signature]

**Cheo:** RM

**Tarehe:** 31/01/2022

**Shahidi:**

**Jina:** EDWARD SIRONGA

**Sahihi:** [signature]

**Cheo:** DM

**Tarehe:** 31/01/2022

MENEJA WA RUWASA
MARA

**KWANIABA YA MWAJIRIWA (FUNDI)**

**Jina:** PATROBERT MAGEGE

**Sahihi:** [signature] PATROBERT MAGEGE P.O.Box 898

**Cheo:** FUNDI KIONGOZI

**Tarehe:** 31/01/2022

**Shahidi:**

**Jina:** David Magenge

**Sahihi:** [signature]

**Cheo:** fundi

**Tarehe:** 31/01/2022

## SCHEDULE OF MATERIALS FOR CONSTRUCTION OF 7 WATER POINTS AND CHAMBERS AND KIOSK FOR BUGOJI/KABURABURA/KANDEREMA WATER SUPPLY PROJECT

| SN | ITEM DESCRIPTION | UNIT | QTY | RATE (TZS) | AMOUNT (TZS) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Site clearance and removal organic layer | m2 | 88 | 500.00 | 44,000.00 |
| 2 | Construction of domestic water points (DPs) including soakaway pit and meter chamber as per drawing No. RUWASAMARA/DP/01 | No | 7 | 300,000.00 | 2,100,000.00 |
| 3 | Plumbing works for DPs as per drawing No. RUWASAMARA/DP/01 | No | 7 | 20,000.00 | 140,000.00 |
| 4 | Construction of inline valve chamber as per drawing. | No | 4 | 60,000.00 | 240,000.00 |
| 5 | Construction of in bulk meter chamber as per drawing No. RUWASAMARA/DP/01 | No | 1 | 120,000.00 | 120,000.00 |
| 6 | Curing as per Project Manager instruction | day | 14 | 7,000.00 | 98,000.00 |
| 7 | Construction of water kiosk including soakaway pit and meter chamber as per drawing | Nr | 1 | 1,700,000.00 | 1,700,000.00 |
| 8 | Transportation of construction materials (Sand,cement,aggregates and blocks) to construction area | Ls | 1 | 300,000.00 | 300,000.00 |
| 9 | Cost for fetching and supplying of water for construction | Ls | 1 | 300,000.00 | 300,000.00 |
| | **Total** | | | | **5,042,000.00** |

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

**MINISTRY OF WATER**

RURAL WATER SUPPLY AND SANITATION AGENCY

RUWASA – Musoma District, P.O Box 738, Musoma,
**Phone** +255738185341, **Website:** www.ruwasa.go.tz,
**E-Mail:** musomadm@ruwasa.go.tz

RUWASA
Rural Water Supply and Sanitation Agency

In reply please quote Ref.No. MA.2/252/01/81

**QUATATION FORM FOR CONSTRUCTION OF 7 WATER POINTS AND 1 WATER KIOSK FOR KANDEREMA AND BUGOJI VILLAGE**

MS PATROBERT MAGEGE
BOX 898, MUSOMA

Please, quote/insert your competitive price for all items mentioned below.

| Sn | ITEM DESCRIPTION | UNIT | QUANTITY | RATE (TZS) | AMOUNT(TZS) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Site clearance and removal organic layer @9m2 for DP and @25 for water kiosk | m2 | 88 | 500 | 44.000/= |
| 2 | Construction of domestic water points (DPs) including soak away pit and meter chamber as per drawing No. RUWASAMARA/DP/01 | No | 7 | 300.000 | 2,100,000/= |
| 3 | Plumbing works for DPs and water kiosk as per drawing. | No | 7 | 20.000/= | 140.000/= |
| 4 | Construction of inline valve chamber as per drawing. | No | 4 | 60.000/= | 240.000/= |
| 5 | Construction of in bulk meter chamber as per drawing No. RUWASAMARA/DP/01 | No | 1 | 120.000 | 120.000/= |
| 6 | Curing as per Project Manager instruction | day | 14 | 7000 | 98,000/= |
| 7 | Construction of water kiosk including soak away pit and meter chamber as per drawing | Nr | 1 | 1,700,000 | 1,700,000/= |
| 8 | Transportation of construction materials (Sand, cement, aggregates and blocks) to construction area | Ls | 1 | 300.000 | 300.000/= |